

Masharti ya Kustahiki Chakula cha Msingi: Nini Unahitaji Kujua ili Kuhifadhi Ruzuku zako

Basic Food Eligibility Requirements: What You Need to Know to Keep Your Benefits

Ruzuku zako zimewekewa kikomo cha muda maalum ikiwa hufanyi kazi

Tunakuzingatia wewe kuwa ni Mtu mzima Mwenye Afya Njema bila ya Wategemezi (ABAWD) kwa Chakula cha Msingi kwa sababu una uwezo wa kufanya kazi na huna watoto katika kaya yako,

Unaweza kupokea ruzuku za Chakula cha Msingi kwa miezi mitatu kila baada ya miezi 36 ikiwa hutimizi masharti ya kazi.

Jinsi gani ya kuhifadhi ruzuku zako za chakula cha msingi

Lazima ufanye moja au zaidi ya shughuli zifuatazo ili kuhifadhi ruzuku zako kwa zaidi ya miezi mitatu:

- Kamilisha kazi ya kujitolea kupitia programu ya Workfare kila mwezi. Kiwango cha ruzuku zako za kila mwezi huamua idadi ya masaa unayotakiwa kujitolea ili kuhifadhi ruzuku zako za chakula.
- Fanyakazi angalau masaa 20 kwa wiki au masaa 80 kwa mwezi kwa wastani.
- Shiriki katika ajira iliyothibitishwa na jimbo au katika programu ya mafunzo kama vile:
 - Ajira ya Chakula cha Msingi na Mafunzo (BFET). Kwa maelezo zaidi nenda kwenye www.dshs.wa.gov/bfet;
 - Programu zilizojumuishwa katika Ubunifu wa Wafanyakazi na Sheria ya Kazi (WIOA). Kwa maelezo zaidi nenda kwenye <https://www.dshs.wa.gov/esa/community-services-offices/wioa>;
 - AmeriCorps VISTA; au
 - Njia ya Wenyewe Ustadi Mdogo wa Kiingereza (LEP).

Vikwazo vya kushiriki

Wasiliana nasi ikiwa huwezi kushiriki angalau masaa 80 kwa mwezi kwa sababu wewe ni:

- Mlemavu wa kimwili au kiakili;
- Unapokea ruzuku kutoka kwa Idara ya Kazi na Viwanda (L&I), Idara ya Askari Wastaafu, au bima binafsi ya ulemavu;
- Unaishi katika mazingira ambayo yanazuia ajira, kama vile kutokua na makazi kwa muda mrefu;
- Unamtunza mtu ambaye hawezi kujitunza mwenyewe kwa sababu ya umri au ulemavu;
- Unashiriki katika matibabu tegezi ya kemikali au programu ya kuwezesha kuishi upya;
- Umeomba au unapokea ruzuku za kutokua na ajira;
- Umejiandikisha shule angalau nusu muda; au
- Unapokea ruzuku za Msaada wa Fedha taslimu wa Wakimbizi au Fedha za Msaada wa Wenzi.

Mambo ambayo lazima uripoti

Lazima utueleze ikiwa:

- Huwezi kukamilisha idadi inayotakiwa ya masaa ya ushiriki kwa mwezi.
- Kazi yako ipo chini ya masaa 20 kwa wiki.
- Kipato cha kaya yako kipo nje ya kikomo kwa mujibu wa WAC 388-478-0060.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu masharti ya ABAWD katika www.dshs.wa.gov/abawd.

Tupigie kwa nambari 1-877-501-2233 ikiwa una maswali, unahitaji msaada wa kujiunga na programu ya mafunzo, au unahitaji kuripoti mabadiliko.

Unaweza kutembelea katika www.washingtonconnection.org ili kufanya maombi ya ruzuku, kutuma maoni, au kuripoti mabadiliko.